**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Simu: 026 -2961500/1
Nukushi: 026-2961502

OFISI YA RAIS,
IKULU,
1BARABARA YA JULIUS
NYERERE
CHAMWINO
S.L.P. 1102,
40400 DODOMA.

## TAARIFA KWA UMMA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mamlaka aliyonayo chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Tume za Uchunguzi, Sura ya 32, ameunda Tume Huru ya kufanya uchunguzi wa matukio ya uvunjifu wa amani yaliyotokea nchini wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025.

Aidha, Mhe. Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu Mstaafu wa Mahakama ya Tanzania ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume hiyo na wajumbe walioteuliwa ni wafuatao:-

(i) Mhe. Profesa Ibrahim Hamis Juma - Jaji Mkuu Mstaafu wa Mahakama ya Tanzania;

(ii) Balozi Ombeni Yohana Sefue - Mwanadiplomasia na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu;

(iii) Balozi Radhia Msuya - Mwanadiplomasia na Balozi Mstaafu;

(iv) Balozi Lt. Gen. Paul Meela - Mwanadiplomasia na Balozi Mstaafu;

(v) IGP (Mstaafu) Said Ally Mwema - Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania Mstaafu;

(vi) Balozi David Kapya - Mwanadiplomasia na Balozi Mstaafu; na

(vii) Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax – Aliwahi kuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Imetolewa na Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi,

*Balozi Dkt.* Moses M. Kusiluka
**KATIBU MKUU KIONGOZI**
18 Novemba, 2025